JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

(SURA YA 413)

KANUNI

*Zimetungwa chini ya Kifungu cha 45(2)(i)*

# KANUNI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MATUMIZI YA MFUMO WA UFUATILIAJI MWENENDO WA VYOMBO VYA USAFIRI ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

### SEHEMU YA KWANZA
### VIFUNGU VYA AWALI


1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.


### SEHEMU YA PILI
### IDHINI KWA WASAMBAZAJI


4. Maombi ya cheti cha idhini ya kusambaza vifaa
5. Vigezo vya kumuidhinisha msambazaji
6. Kufanya majaribio ya vifaa
7. Idhini kwa msambazaji wa vifaa
8. Cheti cha idhini
9. Kuhuisha cheti cha idhini
10. Kusimamisha cheti cha idhini

SEHEMU YA TATU
MASHARTI KWA MSAMBAZAJI WA VIFAA

11. Masharti kwa msambazaji wa vifaa
12. Masharti kwa mtoa huduma

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA UJUMLA

13. Vifaa visiathiri utendaji kazi wa chombo
14. Makosa na adhabu
15. Mapitio
16. Rufaa

MAJEDWALI

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

(SURA YA 413)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 45(2(i))*

## KANUNI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MATUMIZI YA MFUMO WA UFUATILIAJI MWENENDO WA VYOMBO VYA USAFIRI ZA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Matumizi ya Mfumo wa Ufuatiliaji Mwenendo Wa Vyombo vya Usafiri za Mwaka 2023

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa wasambazaji wa vifaa vya ufuatiliaji mwenendo wa vyombo vya usafirishaji pamoja na watoa huduma wa usafirishaji katika masuala ya ufuatiliaji wa mwenendo wa vyombo kwa Tanzania Bara.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo;:

Sura 413

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4(1) cha Sheria;

"Programu ya maombi kutambuana" kwa kifupi "API" maana yake ni namna ambayo program za kompyuta mbili tofauti au Zaidi zinaweza kuwasiliana kwa pamoja;

Sura. 130

"Mamlaka ya Viwango" maana yake ni Mamlaka ya Viwango na Ubora ya Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Ubora;

"Kifaa cha Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Chombo" kwa kifupi "VTD'' maana yake ni kifaana viunganishi vyake vinavyounganishwa kwenye chombo cha umma chenye uwezo wa kutunza kumbukumbu na kuhamisha taarifa za muda huo kwenye mfumo;

"Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Chombo" kwa kifupi "VTS" maana yake ni mfumo unaopokea, kutunza, kufuatilia na kuonesha kwa wakati mwenendo wa chombo cha usafiri wa umma;

"Msambazaji" maana yake ni kampuni iliyosajiliwa au taasisi ya serikali inayoshughulika na kusambaza na kufunga vifaa VTD's;

T.S 76 ya 2020

"mtoa huduma" maana yake ni mtu au kampuni iliyosajiliwa kama mmiliki wa chombo cha moto chini ya Kanuni za Leseni za Usafirishaji za magari ya kubeba Abiria kwa kutoa huduma zinazodhibitiwa;

"Mfumo unaotumika duniani kwa mawasiliano" kwa kifupi "GSM" maana yake ni ni mtandao unatumika na mitandao ya simu kwa kiasi kikubwa duniani kwa kuhamishia taarifa.

## SEHEMU YA PILI
## IDHINI KWA WASAMBAZAJI

Maombi ya cheti cha idhini cha kusambaza vifaa

4. (1)Mtu anayetaka kusambaza na kuweka VTD kwenye chombo cha usafirishaji anatakiwa aombe idhini kwa Mamlaka kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika Jedwali la kwanza la Kanuni hizi na kulipa ada ya maombi iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(2) Maombi chini ya kanuni ndogo ya (1) yataambatishwa na-

a) nakala ya cheti cha usajili wa kampuni;
b) nakala halali ya leseni ya biashara;
c) nakala ya hati miliki au nakala ya mkataba wa pango wa ofisi;
d) nakala halali ya cheti cha mlipa kodi; na
e) sampuli ya VTD inayotarajiwa kufungwa.

Vigezo vya kumuidhinisha msambazaji

5. Mamlaka inaweza kumuidhinisha msambazaji wa vifaa chini ya kanuni hizi baada ya kutimiza vigezo vifuatavyo-

a) Msambazaji ni kampuni iliyosajiliwa Tanzania au Taasisi ya Serikali;
b) Msambazaji anatoa nyaraka za kiufundi ya vifaa kwa ajili ya kuchukua kumbukumbu na kuchakata taarifa inayopelekwa VTS;
c) Msambazaji ana vifaa ambavyo-
    (i) Vina uwezo wa kuchukua kumbukumbu, kutunza na kuhamisha taarifa kwa muda huohuo;
    (ii) Vina viwango vilivyowekwa na Mamlaka ya Viwango;
    (iii) Havina athari katika uendeshaji wa chombo cha usafirishaji;
    (iv) Vina uwezo wa kuchukua kumbukumbu na kuhifadhi matukio au taarifa hata kusipokuwa na mtandao na taarifa hizo kusoma pindi mtandao utakaporudi;
    (v) Vina uwezo wa kutuma taarifa kwa mfumo Mamlaka wa ufuatiliaji mwenendo wa chombo;
    (vi) Vina uwezo wa kutuma GPS kwa muda mahsusi;
    (vii) Visishindwe kufanya kazi hata pale vifaa vitakapokuwa vimechomoka kutoka kwenye umeme au pale alama ya mwendo itakapokuwa imechomoka isiweze kwenda kwa mwendo uliopitiliza;
    (viii) Vinawezeshwa kuwa na namna ya kukubali vifaa vya nje na kuweka muunganisho wa sehemu ya majaribio ya vifaa na uhakiki wa utendaji kazi wa vifaa hivyo;
d) Msambazaji ana wafanyakazi wenye ujuzi wa kutosha wa kuunganisha and kuvihudumia vifaa vya ufuatiliaji wa mwenendo wa vyombo;

e) Msambazaji awasilishe kwa Mamlaka Ceti cha Uthibitisho cha Mtengenezaji wa Vifaa na uthibitisho wa waranti ya japo mwaka moja kwa vifaa hivyo;

f) Msambazaji anatekeleza maelekezo yaliyopo kwenye Jedwali la Pili baada ya majaribio chini ya Kanuni hizi; na,

g) Msambazaji amelipa ada stahiki kama zilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

Majaribio ya Utendaji kazi wa VTD

6. Baada ya kupokea maombi, Mamlaka itamtaka Msambazaji kufunga kifaa kwenye chombo kwa ajili ya majaribio.

Idhini kwa msambazaji wa VTD

7. (1) Mamlaka inaweza kumuidhinisha Msambazaji kusimamia vifaa ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea maombi endapo itaridhika na vigezo vya msambazaji chini ya kanuni ya tano na majibu ya majaribio ya utendaji kazi wa VTD.

(2) Mamlaka inaweza kukataa kumuidhinisha msambazaji wa VTD kama-

(a) Mwombaji atashindwa kukidhi vigezo vya kanuni ya tano;

(b) Mwombaji amejihusisha na vitendo vya kukosa uaminifu au uongo;

(c) Mwombaji atashindwa kulipa ada stahiki; na,

(d) VTD ya mwombaji itashindwa kufaulu majaribio chini ya kanuni ya 6.

(3) Endapo Mamlaka itakataa kutoa idhini kwa msambazaji inaweza kumuagiza mwombaji kurekebisha mapungufu yaliyobainika na kurudisha kwa Mamlaka ndani ya siku kumi na nne.

(4) Endapo mwombaji atashindwa kufanya marekebisho ndani ya siku thelathini tangu kukataliwa kupewa idhini, atatakiwa kuwasilisha maombi mapya.

Cheti cha idhini

8. (1) Mamlaka itatoa cheti cha idhini kwa msambazaji wa VTD aliyeidhinishwa.

(2) Cheti cha idhini kitakuwa halali kwa kipindi cha miaka mitatu na kinaweza kuhuishwa.

(3) Msambazaji aliyeidhinishwa atatakiwa kulipa ada stahiki kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

Kuhuisha cheti cha idhini

9. (1) Mmliki wa cheti cha idhini anapaswa kuwasilisha maombi ya kuhuisha cheti ndani ya siku thelathini kabla ya cheti chake kuisha muda wake kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

(2) Maombi ya kuhuisha yataambatishwa na nyaraka zifuatazo-

(a) Nakala ya leseni ya biashara;

(b) Nakala halali ya cheti cha mlipa kodi; na,

(c) Nakala ya hati miliki au mkataba wa pango wa ofisi kama kuna mabadiliko.

(3) Mamlaka inaweza kuhuisha cheti cha idhini baada ya kupokea maombi ya kuhuisha chini ya Kanuni hizi.

Kusimamisha cheti cha idhini

10. (1) Mamlaka inaweza kusimamisha au kufuta cheti cha idhini cha msambazaji baada ya kutokea yafuatayo-

a) Uthibitisho wa msambazaji kujihusisha na vitendo vya kuondoa uamninifu au uongo;
b) Kushindwa kurekebisha kifaa kisichofanya kazi ndani ya masaa ishirini na nne;
c) Uthibitisho wa kutoa taarifa za uzushi au zinazopotosha;
d) Uthibitisho wa kujihusisha na uchezeaji wa VTD;
e) Uthibitisho wa kuwepo na madhaifu ya VTD; na
f) Uthibitisho wa kuvunja mashari au kanuni yoyote katika kanuni hizi.

(2) Sababu za kusimamisha au kufuta cheti cha idhini zinaweza kutumika kuondoa sifa wakati wa maombi ya kuhuisha idhini.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA KUSAMBAZA VIFAA

Masharti kwa msambazaji wa VTD

11. Msambazaji wa VTD atatakiwa-

a) Kusambaza and kufunga vifaa kwenye chombo cha mtoa huduma kwa kumuuzia au kumuazimisha;
b) Kuwepo kwa huduma za matengenezo ya vifaa vilivyosambazwa ndani ya masaa ishirini na nne tangu kutokea au kupata taarifa ya kuharibika kifaa;
c) Kuandaa namna ya kuunganisha vifaa na mfumo wa VTS kwa kutumia API au kwa njia nyingine itakayokubalika;
d) Kuhakikisha kuwa VTD inaendelea kutuma taarifa VTS;
e) Kuendana na matakwa ya vipimo maalum vya VTD vitakavyo ainishwa na Mamlaka;
f) Kutoa mafunzo ya matumizi ya VTD kwa watoa huduma na wadau wengine;
g) Kuwezesha Mamlaka kupata VTD pale inapohitajika;
h) Kuhakikisha kuwa taarifa za mtoa huduma zinazopatikana hazitolewi kwa mtu mwingine bila kupata idhini ya Mamlaka;
i) Kuhakikisha kuwa VTD ziko salama na vinaunganishwa kwa namna ambayo hataruhusu kirahisi kuchezewa moja kwa moja au vinginevyo;
j) Kuhakikisha kuwa mafundi wana vaa sare na vitambulisho wanapokuwa kazini;
k) Kutomkatia huduma mtoa huduma bila kupa taarifa ndani ya siku thelethini kwa Mamlaka; na,
l) Kuingia kwenye mkataba na mtoa huduma kabla ya kumuwekea VTD.

Masharti kwa mtoa huduma

12. Mtoa huduma atahakikisha kuwa-

a) VTD inayounganishwa katika chombo chake imefanywa na msambazaji aliyeidhinishwa na Mamlaka;

b) VTD inatunzwa dhidi ya mazingira hatarishi, kuchezewa na kina kinafanya kazi muda wote;
c) Ikitokea kutokufanya kazi au kuharibika kwa VTD itolewe taarifa nani ya masaa mawili kwa msambazaji na kama haijafanyiwa kazi atoe taarifa kwa Mamlaka ndani ya masaa kumi na mbili tangu ulipotokea uharibifu; na,
d) Kumruhusu msambazaji au Mamlaka kufanya ukaguzi wa VTD bila kuzuiwa.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA UJUMLA

VTD isiathiri utendaji kazi wa chombo

13. - (1) Uwekaji wa VTD hautakiwa kuathiri utendaji kazi wa chombo cha usafirishaji.

(2) Uharibifu wowote utakaosababishwa na ufungaji wa VTD utatakiwa kulipwa na msambazaji.

Makosa ya jumla

14. Mtu atakaye fanya kinyume kifungu chochote cha Kanuni hizi, atakuwa amefanya kosa na ataadhibiwa kwa faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki tano lakini isizidi milioni moja au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisischozidi miaka miwili.

Mapitio

T.S. 73 ya 2020

15. Mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Mamlaka chini ya Kanuni hizi anaweza, ndani ya siku kumi na nne kutoka siku ya maamuzi, ataomba kufanya mapitio, kwa mujibu wa Kanuni ya Mamlaka ya Udhibiti Usafari Ardhini Utaratibu wa Mapitio

Rufaa
Sura ya 285

16. Mtu ambaye hajaridhishwa na maamuzi ya Bodi anaweza kukata rufaa Baraza la Tume ya Ushindani.

**MAJEDWALI**

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya kanuni 4(1) na 9(1)

FOMU YA MAOMBI

1.Aina ya maombi / Weka alama ya pata katika sanduku husika

| | |
|---|---|
| Mpya | |
| Kuhuisha | |
| Kurudufu | |

2.TAARIFA ZA MWOMBAJI WA CHETI

Jina kamili la Mwombaji …………...........................................................
(Jina/Kampuni/Mshirika – kwa HERUFI KUBWA)
Anwani ……………………………………......………
Simu ya Ofisi/Simu ya kiganjani: …………………………………….….
Simu ya kiganjani ya Mwombaji:...……………………………..……..
Barua pepe: ……………………………………..…………………

Anwani ya Makazi:
Mtaa: ……………………………….…….
Namba ya Kitalu: ………………………..…..
Namba ya ofisi: ......................................
Namba ya kitalu ……………………………
Ushawahi kuwa na maombi yaliyokataliwa, kusimamishwa au kufutiwa
Ndiyo:…..
Hapana:……
Kama ndiyo eleza sababu za kukataliwa, kusimamishwa au kufutiwa maombi
………......................................................................……….

3. KIAPO

Mimi /Sisi tunaapa kuwa taarifa zilizotolewa ni za kweli kwa ufahamu wangu/wetu wote

Jina Kamili: ………………………………... Sahihi: ………………………...

Cheo: ……………………………… Tarehe: ……………………………..

TAHADHARI:

Ijulikane kuwa kutoa taarifa ya uongo ili kupata cheti kilichoidhinishwa ni makosa ambayo yanaweza kuadhibiwa kwa faini au kifungo.
Wasilisha taarifa kwa Mamlaka ikitokea mabadiliko yoyote kwenye taarifa zilizopo kwenye fomu hii, kutokufanya hivyo ni makosa chini ya Kanuni hizi.

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

NAMBA YA JALADA LA MMILIKI

……….........................................

Uhakiki na Idhini
(a) Haijaidhinishwa:
Weka sababu
………………….......………
(b) Imeidhinishwa:
Tarehe ya kuanza:
………………………………….
Tarehe ya kuisha:
……………………......

Jina kamili la Afisa:
……………………………………………………………..
Cheo:
………………………………..
Sahihi:
…………………………………..
Tarehe:
…………………………………
Kiasi kilicholipwa: …………………………….. Namba ya stakabadhi. ……………………..

Tarehe:...………………………… Sahihi: ……………………….

ANGALIZO: VIAMBATISHO

1. Maombi ya kwanza yataambatishwa na vifuatavyo:
(a)nakala ya cheti cha usajili wa kampuni;
(b)nakala ya leseni ya biashara;
(c)nakala ya hati miliki ya eneo au mkataba wa pango wa ofisi;
(d) nakala ya cheti cha mlipa kodi;
(e) nakala ya kitambulisho cha Utaifa kwa mtu wa kawaida.

2. Kuhuisha

(a) uthibitisho wa malipo ya levi ya Mamlaka kwa mwaka ulioisha;
(b) nakala ya leseni ya biashara;
(c) nakala ya cheti cha mlipa kodi; na,
(d) nakala ya hati miliki ya eneo au mkataba wa pango wa ofisi kama kuna mabadiliko

JEDWALI LA PILI

*Limetengenezwa chini ya 5(f)*

MAELEZO YA UTEKELEZAJI

| S/N | Compliance Statement/Technical Specification | | Indicate whether Comply or Not Comply | Remarks (if any , Evidence or explanations on how the compliance will be achieved or not) |
|---|---|---|---|---|
| 1.0 | | General Attributes | | |
| 1.1 | Provide and Install fixed Vehicle tracking devices to transporters by either selling, leasing or hiring to them | | | |
| 1.2 | Provide maintenance services to the fixed tracking devices sold ,leased or hired to transporters | | | |
| 1.3 | Prepare a middleware or an integrating mechanism with LATRA VTS platform using given API or another agreed mechanism | | | |
| 1.4 | Comply with ALL requirements as specified in the API or another agreed mechanism. | | | |
| 1.5 | Provide a mechanism / interface where LATRA can directly interrogate and manage on real time the tracking device and update some parameters such as speed limit at any time | | | |
| 1.6 | Ensure that GPS data transmitted to LATRA VTS platform is complete, correct and accurate | | | |
| 1.7 | Inform LATRA of the availability of new Technology on Tracking System and devices from Time to time | | | |
| 1.8 | Ensure there is NO TAMPERING of the fitted tracking device | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1.9 | Ensure that fitted tracking devices are transmitting to LATRA VTS Application 24/7 | | | |
| 1.10 | Report immediately to LATRA of any event that could lead to the tracking device not working properly (such as accident, theft etc.) | | | |
| 1.11 | Ensure compliance with standards specifications of the fixed tracking devices as set by LATRA including integration to the system using the API provided by LATRA under annexure-1 | | | |
| 1.12 | Provide Training on the use of fitted tracking devices to Transporters and other Stake holders | | | |
| 1.13 | Provide access and information to LATRA at any given time for the GPS data receiving, integration/ middleware platform for auditing and quality assurance purposes | | | |
| 1.14 | Settle GPS/GPRS communication charges claim made by the client within seven days from submission of such claim | | | |
| 1.15 | Provide GPS positioning values | | | |
| 1.16 | Provide Alerts information | | | |
| 1.17 | Updating of GPS values for at least every 3 min | | | |
| 1.18 | Storing of alerts information while disconnected from GSM network and updating back to central server upon connection to GSM network | | | |
| 1.19 | Provide Low battery alerts | | | |
| 1.20 | Provide alerts on Lost connection with tracking units | | | |
| 1.21 | Provide damage alerts from tracking units | | | |
| 1.22 | API provided or any other agreed integration mechanism may be changed or updated by LATRA from time to time depending on the need, or change in technology, which may lead for you (the bidder) to change immediately the way you integrate or communicate with VTS at no cost to LATRA. | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1.23 | Submit of Complete documentation of the tracking devices (including all associated protocols) Applicable for non BSMART devices | | | |
| 2.0 | | Specific events/ attributes to be sent to the VTS platform | | |
| 2.1 | Vehicle Registration Number | | | |
| 2.2 | Driver's Name (Driver Identification such as use of i-Button or similar) | | | |
| 2.3 | Latitude (in decimal degrees) | | | |
| 2.4 | Longitude (in decimal degrees) | | | |
| 2.5 | Altitude (in meters above sea level) | | | |
| 2.6 | GPS timestamp (YYYY-MM-DD HH:MM:SS) | | | |
| 2.7 | Speed (km/h) | | | |
| 2.8 | Bearing (Direction In degrees) | | | |
| 2.9 | Odometer (KM) | | | |
| 2.10 | Satellite count (Receivable number of satellites) | | | |
| 2.11 | HDOP (Horizontal Dilution of Precision-Quality of signal) | | | |
| 2.12 | RSSI (Received Signal Strength Indication) | | | |
| 2.13 | LAC (Local Area Code) | | | |
| 2.14 | Cell ID (Cell ID) | | | |
| 2.15 | MCC (Mobile Country Code) | | | |
| 2.16 | IMEI (International Mobile Equipment Identity) | | | |
| 2.17 | Data Received Time (Time Received by Server – YYYY-MM-DD HH:MM:SS) | | | |
| 2.18 | Data Process Time (Time insert into Database – YYYY-MM-DD HH:MM:SS) | | | |
| 2.19 | MSG_ID (Unique data running number-64bits) | | | |
| 3.0 | | Vehicle specific activities for each event sent to the VTS | | |
| 3.1 | Movement/Logging (Default) | | | |
| 3.2 | Engine ON | | | |
| 3.3 | Engine OFF | | | |
| 3.4 | Speeding | | | |
| 3.5 | Hash Braking | | | |
| 3.6 | Hash Turning | | | |
| 3.7 | Hash Acceleration | | | |
| 3.8 | Panic Button (Driver's Side) | | | |
| 3.9 | Internal Battery Low | | | |
| 3.10 | External Battery Disconnected | | | |
| 3.11 | Excessive Idle | | | |
| 3.12 | Accident | | | |
| 3.13 | Panic Button (Passenger Side) | | | |
| 3.14 | Device Tempering | | | |
| 3.15 | Black box Data logging | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3.16 | External Power Voltage | | | |
| 3.17 | Device Internal Battery Voltage | | | |
| 3.18 | Black Box Data logging | | | |
| 3.19 | Fuel data report | | | |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni 4(1), 5(g) na 8(3))*

ADA

| Na. | Aina | Shs. | US $ |
|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya Maombi | 100,000 | 50 |
| 2 | Ada ya Cheti cha Idhini | 5,000,0000 | 5,000 |

Dodoma,
..........................., 2023

MAKAME M. MBARAWA
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*